**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI**
**MAMLAKA YA VITAMBULISHO VYA TAIFA**

# HOTUBA YA MHE. MKUU WA WILAYA YA MBARALI KWA VYOMBO VYA HABARI; UZINDUZI WA ZOEZI LA UTOAJI VITAMBULISHO VYA TAIFA KWA WATUMISHI WA UMMA MKOA WA MBEYA- 27 MACHI 2017

Imewasilishwa na:
Mhe. Mkuu wa Wilaya,
Mbarali,
**MBEYA.**

**Ndugu Katibu Tawala Wilaya,**

**Kamati ya Ulinzi na Usalama Wilaya,**

**Wakuu wa Taasisi na Idara za Serikali,**

**Wafanyakazi na Watendaji wote wa Serikali,**

**Watumishi wa NIDA mlipo hapa,**

**Ndugu Waandishi wa Habari,**

**Wageni Waalikwa Mabibi na Mabwana.**

**Utangulizi:**

Awali ya yote nichukue fursa hii kumshukuru Mungu kwa kutujalia afya njema leo tunapokutana kwenye sherehe fupi ya uzinduzi wa utoaji Vitambulisho vya Taifa kwa Watumishi wa Umma baada ya kukamilisha taratibu zote za usajili.

Mkoa wa Mbeya na hasa Wilaya ya Mbarali ni miongoni mwa Wilaya zilizokamilisha zoezi la Usajili na Utambuzi wa Watumishi wa Umma, na kwa mujibu wa NIDA tayari taarifa za watumishi wote waliosajiliwa zimeshaingizwa kwenye mfumo wa mishahara wa Utumishi Serikalini na hivyo leo tunashuhudia kukamilika kwa zoezi hilo hatua ya mwisho ambayo ni utoaji wa Vitambulisho.

Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa ilifika kuripoti hapa Wilayani tarehe **20/9/2017** na kwa matayarisho ya kuanza kwa zoezi hili la kuwasajili watumishi pamoja na kufungua ofisi yao ya kudumu, zoezi ambalo tumeshuhudia likifanyika kasi ya pekee kusambaza vifaa pamoja na kuanza utekelezaji wa zoezi la Usajili na Utambuzi lililoanza rasmi Kitaifa tarehe 03/10 na kumalizika tarehe 31/10/2016.

**Ndugu wageni waalikwa,**

Moja ya kichocheo kikubwa cha mafanikio ya zoezi hili kwa Wilaya yetu ni ari, moyo wa kujituma na kufanya kazi kwa watumishi wa NIDA, watendaji na viongozi kwa jumla; na kuchukulia zoezi hili kwa uzito mkubwa kama ulivyokuwa mwongozo wa Serikali chini ya Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Nichukue fursa hii kuwapongeza sana watumishi wote wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa mlilopangiwa kufanya kazi hapa Mbarali, kwa kazi nzuri, kujituma pamoja na mazingira ya ugeni na changamoto za hapa na pale katika kuendesha zoezi hili, lakini mlifanikisha na kukamilisha zoezi hili kwa wakati.

Nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitawashukuru na kuwapongeza watumishi wote mlioshiriki zoezi hili kwani kupokea kwenu zoezi hili kwa moyo mnyofu na kutoa ushirikiano kwa watumishi wetu wa NIDA kumekuwa chachu ya kufanya vizuri si tu Wilaya yetu lakini mkoa mzima na kufikia malengo tuliyojiwekea.

Endapo kuna mfanyakazi yeyote ambaye kwa namna moja au nyingine hakusajiliwa katika zoezi hili, wito wangu afike kwenye ofisi ya NIDA iliyofunguliwa katika Wilaya yetu kujisajili na kuhakiki taarifa zake kwani kushindwa kufanya hivyo ni hasara yake kwa baadae. Mfumo wa Vitambulisho vya Taifa umeunganishwa na mfumo mkuu wa Utumishi na hivyo

iwapo taarifa zako zitakosekana katika mfumo wa NIDA, hivyo kukosekana kwa taarifa zako kwenye mfumo huo kutakusababishia usumbufu na hata kukosa stahiki zako.

**Ndugu wageni waalikwa;**

Hatua tuliyofikia leo ni kubwa na ya kujivunia kama Wilaya, na hivyo nitoe rai kwa wananchi wote, wageni na wakimbizi wanaoishi kihalali hapa kwetu kujiandaa na hatua ya pili ya usajili ambayo inaanza mara moja na katika baadhi ya Kata zoezi hili la kuwasajili wananchi limeanza, sambamba na kuwasajili wageni wote wanaoishi kwenye Wilaya yetu.

Zoezi hili litahusisha Raia wote wenye umri wa miaka 18 na kuendelea, Wageni wanaoishi kihalali hapa nchini na Wakimbizi.

Ofisi ya NIDA itatupa utaratibu mzuri wa namna itakavyoendesha zoezi hilo katika Wilaya ya Mbarali na makusudio ni kuwasajiliwa zaidi ya wananchi **187,106**.

Nitoe rai kwa wananchi wote wa Wilaya ya Mbarali, kuandaa Viambatisho msingi vinavyohitajika kuthibitisha umri, makazi na uraia ambavyo ni Cheti cha kuzaliwa, Pasipoti (passport) Hati ya kusafiria, vyeti vya shule, kadi ya kupigia kura, kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi, TIN namba, Bima ya Afya, mfuko wa Hifadhi ya Jamii. Kuwa na viambatisho vingi ni kutambulika kwa haraka zaidi. Nimevitaja viambatisho hivi kila mmoja aanze kujiandaa na pindi zoezi linapokufikiwa iwe rahisi kukamilisha zoezi hili kwa wakati.

Ikumbukwe ili kukamilisha hatua zote za msingi za usajili ni lazima Uhakiki wa taarifa kufanywa; na hatua hii inahusisha kamati za Ulinzi na Usalama za Vijiji na Mitaa sambamba na wananchi kupewa fursa ya kuwawekea mapingamizi wale wote ambao wanawatilia mashaka uraia wao. Nitoe rai kwa watendaji wote kuanzia ngazi ya Wilaya, Tarafa, Kata, Mtaa na Vijiji, zoezi hili ni muhimu sana na kila mmoja wenu anawajibika kutoa ushirikiano kwa nafasi yake ili likamilike na kusimamia kwa dhati kuhakikisha hakuna mgeni ambaye atasajiliwa kwa hadhi ya raia. Ndiyo maana tuna vitambulisho vya aina tatu; Raia, Mgeni na Mkimbizi.

Niseme Wilaya ya Mbarali tutashirikiana kwa karibu katika kuhakikisha makundi yote Raia, Wageni na Wakimbizi wanasajiliwa kwa wakati na kila kundi linasajiliwa kuendana na sifa zake; na hakuna mgeni atakayejipenyeza kusajiliwa kupewa kitambulisho cha Raia wakati anajulikana kuwa ni mgeni. Kila kundi litasajiliwa kulingana na sifa zake kwa kufuata taratibu na sheria za Usajili.

**Ndugu wageni waalikwa;**

Kabla sijahitimisha hotuba yangu ni vema nikagusia faida kubwa za Vitambulisho vya taifa. Vitambulisho hivi vina faida nyingi ambazo zimejikita katika sehemu kubwa nne; kiulinzi na kiusalama, kiuchumi, kijamii na kisiasa.

Kwakuwa kitambulisho hiki ni cha mfumo wa kielektroniki (smart card) kinauwezo wa kufanya mambo mengi ikiwa ni pamoja na kuunganishwa na mifumo mingine ya Serikali katika kubadilisha taarifa, mfano mfumo wa vizazi na vifo, Mishara, kodi n.k

Kupitia Kitambulisho hiki wananchi watatambulika kirahisi na hivyo kuwawezesha kupata huduma kwa haraka pamoja na kupata mikopo na pembejeo za kilimo kirahisi kwa kuwa kitambulisho hiki kina jibu maswali makuu nani ni nani? Yuko wapi na ana fanya nini ?

Hii ni fursa ya pekee kwa Taifa Letu, na nafasi ya kila mmoja wetu kuitumia ili kutambulika kama raia halisi wa nchi hii na kunufaika na matunda na nchi yake, Pamoja na kutumia fursa zilizopo kujiletea maendeleo kwa haraka zaidi.

Baada ya kusema hayo; niwapongeze tena wale wote waliofanikisha maandalizi ya sherehe hii fupi na kukamilika kwa zoezi la usajili wa watumishi wa Umma Wilaya ya Mbarali; hatua ambayo inatoa fursa ya kuanza hatua nyingine ya Usajili wa Wananchi. Hongereni sana

Baada ya kusema hayo machache; sasa niko tayari kuzindua zoezi la kuanza kugawa vitambulisho vya Taifa kwa Watumshi wa Umma ambao wamekamilisha taratibu za usajili na kutimiza vigezo vya kupewa Vitambulisho vya Taifa. Asanteni sana kwa kunisikiliza.

**MWISHO**